**11 JUNI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Arobaini na Tano – Tarehe 11 Juni, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wa Kumi na Tano, Kikao cha Arobaini na Tano.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge, aulize swali lake.

Na. 578

**Hitaji la Katibu Muhtasi – Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Sikonge**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaipa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Sikonge Katibu Muhtasi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora kupitia barua ya tarehe 5 Aprili, 2024 imefanya mawasiliano na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ili kujaza nafasi hiyo na tayari Mwandishi Mwendesha Ofisi ameshariporti na kuanza kazi tarehe 8 Aprili, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaendelea kushughulikia vibali vya ajira kwa ajili ya kuajiri na kuwapanga wataalamu mbalimbali kwenye maeneo yenye upungufu kote nchini ukiwemo Mkoa wa Tabora, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu hayo ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza napenda kushukuru maelekezo ya Serikali hasa kuhusu *RAC* kumwagiza Mkurugenzi kumpeleka Mtumishi huyu ambaye anaitwa Maselina Julius ambaye ni Mwandishi Mwendesha Ofisi aliyeripoti tarehe 8 Aprili, 2024 kama ulivyosema, lakini nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba hatua kama hiyo iliwahi kuchukuliwa mwaka 2018 na mtumishi wa aina hiyo kutoka kwa Mkurugenzi akaa katika Ofisi ya *DC* kwa muda wa miezi sita halafu akarudishwa kwa Mkurugenzi na Ofisi ya *DC* ikabaki tupu mpaka mwaka huu tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa je, swali la kwanza tuna uhakika gani sasa safari hii kwamba huyu mtumishi Maselina Julius atahudumu hapo kwa Mkuu wa Wilaya mpaka hapo atakapopekelewa mtumishi mwingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni kwa nini Serikali isifanye uhamisho wa mtumishi wa kudumu katika nafasi hiyo ili ahamishiwe katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Sikonge mapema iwezekanavyo badala mtumishi wa kuazima?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza ni kweli kwamba mtumishi huyo amehamishiwa katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Sikonge na nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali ni kuona kwamba Ofisi za Wakuu wa Wilaya na ofisi nyingine zote zinakuwa na wataalamu wote wanaohitajika angalau kukidhi mahitaji ya huduma zinazolotewa.

Kwa hiyo, huyo aliyepelekwa pale ataendelea kufanya kazi pale, haitatokea kama hiyo iliyotokea mwaka 2018 kwa sababu ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba mtaalamu huyo anafanya kazi hapo na kama anahamishwa basi kunakuwa na mbadala wake ili shughuli ziweze kuendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, kuhusiana na namna ya kuona uwezekano wa kuwapata wataalamu kama hawa, tuna upungufu wa wataalamu hawa lakini Serikali inaendelea kuajiri. Katika kibali cha ajira kinachofuata tutahakikisha maeneo yenye upungufu wataalamu hawa wanapelekwa ili waweze kutoa huduma hizi na yale maeneo ambayo tunahitaji kufanya msawazo wa ndani, tutafanya msawazo wa ndani ili angalau kila ofisi iwe na wataalamu ambao wanahitajika kwa wakati huo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David. Mbunge wa Same Magharibi.

Na. 579

**Kuweka Zege Barabara za Mlimani Same Magharibi**

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuweka zege kwenye barabara za mlimani Jimbo la Same Magharibi ili kuokoa gharama za kuweka vifusi mara kwa mara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiweka zege kwenye barabara mbalimbali kulingana na upatikanaji wa fedha ambapo katika mwaka 2023/2024 Barabara za Makanya – Suji – Mweteni, Saweni – Gavao – Bwambo na Msanga – Chome – Ikokoa zimetengewa shilingi milioni 416.35 kwa ajili ya ujenzi wa barabara za zege zenye urefu wa kilometa 1.6 kwenye maeneo korofi na kazi inaendelea kukamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2017/2018 hadi 2022/2023 *TARURA* Wilaya ya Same imefanya matengenezo ya barabara kwa kiwango cha zege kwenye Jimbo la Same Magharibi yenye urefu wa kilometa 3.55 kwenye maeneo korofi ya barabara za milimani kwa gharama ya shilingi milioni 671.16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha za matengenezo ya barabara kwa kiwango cha zege hasa ukanda wa milimani kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishukuru Serikali kwa kuanzisha mpango huo wa kuweka zege kwenye barabara za milimani kwa sababu wanapoweka vifusi

pindi mvua inaponyesha barabara zile zinazolewa na tunatia hasara Serikali na wananchi wanashindwa kupita, hata hivyo na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Barabara za Msanga – Chome – Ikokoa – Makanya – Tae – Suji na Barabara ya Kisiwani hadi Msindo zina maeneo makorofi mengi sana, je, Serikali haioni kwamba umefika wakati wa kutenga bajeti ya kutosha kusudi barabara hizi zitengenezwe kwa kiwango cha zege ili tuweze ku-*save* hela za Serikali zinazotokana kumwaga vifusi ambavyo vinazolewa na mvua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri ni lini yuko tayari kutembelea Jimbo hili na kuziona hizi Barabara za Chome, Barabara za Makanya – Tae pamoja na Kisiwani – Msindo ili aweze kuona umuhimu wa kutenga fedha za kutosha haraka iwezekanavyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutetea wananchi wake. Kuhusiana na swali lake la kwanza ambalo ameuliza baadhi ya barabara Serikali ina mkakati gani wa kuzijenga kwa tabaka la zege na hasa kwenye maeneo korofi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Msanga – Chome – Ikokoa katika mwaka wa fedha huu wa 2023/2024 zimetengwa shilingi milioni 267.15 kwa ajili ya kujenga meta 100 kwa kiwango cha zege kwenye eneo korofi, lakini pia kwenye eneo hatarishi la Mlima wa Chome imejengwa *strip concrete* ya meta 350, lakini katika mwaka wa fedha ujao 2024/2025 Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 74.9 kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha zege meta 180 kwenye eneo hatarishi la Mlima Ikokoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu Barabara ya Makanya – Tae – Suji Serikali imetenga katika mwaka wa fedha 2024/2025

milioni 161.18 kwa ajili ya kujenga kwa tabaka la zege urefu wa meta 100 kwenye eneo la Mgwasi – Tae, lakini pia ujenzi wa *driffs* nne za meta 32 na kwenye Barabara ya Kisiwani – Msindo, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali ilitumia shilingi milioni 250 kwa ajili ya kujenga meta 500 za *strip concrete*. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuendelea kujenga kwa kiwango cha zege kwenye maeneo hatarishi, kwenye barabara zake hizi ili ziweze kupitika kipindi chote cha mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakaa mimi na yeye tutazungumza, tutapanga ratiba vizuri nipo tayari kutembelea Jimboni kwake kuangalia miundombinu hii ya barabara ili tuweze kuona umuhimu wa kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuzikarabati na kuzijenga vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amar, nilikuona umesimama.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali inaendelea kufungua barabara za mitaa kwenye Makao Makuu ya Wilaya ya Nyang'hwale pale Kharumwa kwa kiwango cha udongo. Je, Serikali ina mpango gani kuziwekea mpango wa kuweka changarawe na baadaye lami hizo barabara za mitaa Kharumwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inaweza kuzihudumia barabara za wilaya kwa kiwango cha lami, lakini kama wote tunavyofahamu tunaanza. Kwa hiyo, tayari Serikali imeanza kuhudumia barabara hizi kwa viwango tofauti ikiwemo viwango vya changarawe, lakini mwisho wa siku hatimaye tunataka barabara zetu zote hizi za wilaya ziwe kwa kiwango cha lami ambacho kitafanya barabara ziweze kudumu kwa muda mrefu na ziweze kupitika mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kutenga fedha kuhakikisha kwamba inaboresha miundombinu ya barabara zetu hizi za wilaya na hususan pia kwenye Jimbo lako Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, nilikuona.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa mwenyekiti, changamoto za barabara za Mlimani kule Same Magharibi zinafanana sana na hali ilivyo kule kwetu Meru na nimeishalisema hapa mara nyingi. Kwa hiyo, sasa niulize Serikali inatoa tamko gani kuhusu barabara za milimani kule Arumeru Mashariki? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge kwa kweli amekuwa akipambania sana suala la Ujenzi wa barabara kwa viwango vitakavyodumu hasa katika Jimbo lake ambalo lina milima. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa sababu tayari tumeshazungumza na suala tayari lipo kwenye michakato na fedha tayari zimeshatengwa, nikuhakikishie Serikali itakuja kujenga barabara, itatenga fedha kila mwaka kuhakikisha kwamba inaboresha miundombinu ya barabara hizi na hasa katika jimbo lako ambalo ni la milima. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Katani, nilikuona.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Luagara kwenda Liponde kilometa 1.5 ilishafanyiwa *feasibility study* na watu wa *TARURA* na walishaweka kwenye bajeti miaka miwili nyuma, ni lini sasa Serikali itakwenda kuweka lami kipande kile?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu barabara hii tayari imeshafanyiwa usanifu na tayari ipo kwenye bajeti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutafuatilia kwa karibu hata baada ya kutoka kwenye maswali hapa tutakaa tutafuatilia kwa karibu ili tuhakikishe kwamba mwaka huu kwa sababu fedha tayari imeishatengwa ili iweze kujengwa barabara hii.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba.

Na. 580

**Ujenzi wa Shule ya Wasichana Arusha**

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI K.n.y. MHE. ZAYTUN S. SWAI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Shule ya Wasichana Arusha ambayo ilipangwa kujengwa katika Kata ya Enkikret – Longido?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia mradi wa kuboresha elimu ya sekondari ilipanga kujenga shule 26 za bweni za wasichana za kitaifa katika mikoa yote nchini. Lengo la shule hizi ni kuongeza fursa kwa wanafunzi wa kike kusoma masomo ya sayansi na kuwaepusha na vishawishi vinavyosababisha kukatisha masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa shule hizi umefanyika katika mikoa yote kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza ilianza kwa mikoa ya Kagera, Shinyanga, Mwanza, Singida, Pwani,

Songwe, Lindi, Dar es Salaam, Njombe na Ruvuma. Aidha, awamu ya pili imefanyika katika mikoa iliyobaki na kufanya mikoa yote kuwa imepokea fedha za ujenzi wa shule za bweni za wasichana za mikoa ikiwemo Mkoa wa Arusha ambapo ujenzi unafanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido na umefikia 85%. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel Shangai.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *okay* kwa kuwa sasa ujenzi wa shule umefikia 85%, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi huo pamoja na nyumba za watumishi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mbunge kwa swali hili zuri sana kwa maslahi ya watoto wote wa kike ambao watasoma kwenye shule hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha mwaka 2023/2024 Serikali itapeleka shilingi bilioni 1.1 katika shule zote zile 16 za wasichana ambazo zilipelekewa shilingi bilioni tatu awamu ya kwanza kwa ajili ya kukamilisha miundombinu ya msingi ikiwemo vyumba vya madarasa kumi, lakini chumba cha TEHAMA kimoja, maktaba moja, nyumba za walimu tatu na mabweni manne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itapeleka fedha hii kwa ajili ya kukamilisha miundombinu ili shule zetu hizi ziweze kuwa zimekamilika na wanafunzi waweze kuingia na kuanza kuzitumia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond nimekuona, baadaye Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naomba unipe fursa nimpongeze sana Rais wa Nchi Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuliona hili kwa ajili ya wasichana. *(Makofi)*

Naomba kuuliza swali je, katika shule hizo zinazoenda kujengwa ambazo ni za sayansi, wamezingatia kutupatia *lab technicians? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamsikia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hujamwelewa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamsikia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally, naomba urudie ili swali kwa ufupi.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za sayansi zinaenda sambamba na kuwa na *laboratories* na *laboratories* hizo zinataka *lab technicians,* lakini naomba kumwuliza Naibu Waziri, je, mmezingatia kutoa au kutuma *lab technicians* wa kutosha kwenye shule hizo mpya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ujenzi wa hizi shule kama nilivyotangulia kusema awali ukiacha majengo tu ya madarasa, lakini kutakuwa kuna chumba cha TEHAMA, kutakuwa na maktaba, nyumba za walimu na mabweni. Kwa hiyo, chumba cha TEHAMA kitakuwepo na kwa sababu msingi ni kuhakikisha kwamba shule hizi zinatoa elimu

iliyobora kwa watoto wa kike, wakati wa kutoa watumishi yaani wakati wa kuajiri na kupanga watumishi kwa ajili ya kuhudumia shule hizi lazima Serikali tutazingatia ili hiki chumba cha TEHAMA kipate matumizi kiwe kina *lab technicians.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, nilimtaja Mheshimiwa Mama Salma ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Rungwe tuna shule nzuri sana ya wavulana. Tunashukuru Serikali kwa kuikarabati ni lini mtatujengea shule ya wasichana katika wilaya hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kujibu kwenye majibu yangu ya msingi shule hizi zipo 26 ziko kwenye Mradi wa *SEQUIP* na kila mkoa inapata shule moja ya wasichana, ya bweni na ni ya sayansi. Kwa hiyo, Mkoa wa Mbeya tayari una shule moja kwa hiyo hatutojenga katika kila kata, ni shule maalum Mheshimiwa Rais amehakikisha ametenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kila mkoa unapata shule hii ya bweni ya wasichana ya sayansi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Salma Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliona hili na kujenga na kutupatia hizo shule 26 katika nchi yetu ya Tanzania na mkoani kwetu Lindi hasa kwenye Jimbo langu kuwa ni miongoni mwa zile shule za kwanza ambazo zimejengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wa kike wanahitaji ulinzi, je, ni lini mtatupatia pesa kwa ajili ya uzio kwa ajili kuwalinda watoto hawa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu amekuwa akitetea sana, sana, sana maslahi ya watoto wa kike kupata elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake kama nilivyotangulia kujibu katika swali la nyongeza hapo awali Serikali italeta na itapeleka shilingi bilioni 1.1 kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha kuisha, mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili ya kukamilisha miundombinu yote ya msingi katika shule hizo ambazo zilipewa fedha katika awamu ya kwanza, kwa sasbabu shule hizi 16 ikiwemo shule ambayo imejengwa Mkoa wa Lindi zilipokea shilingi bilioni tatu awamu ya kwanza na sasa zitapokea mwaka huu shilingi bilioni 1.1 awamu ya pili kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu yote ya msingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab Katimba ahsante sana, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri mwenzio kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 581

**Mkataba wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza: -

Je, ni mikataba mingapi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi ambayo watumishi wake wanatoka Zanzibar?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira imeridhia mikataba 12 ya kimataifa na kikanda kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Utekelezaji wa mikataba hii hufanyika kwa ushirikiano na uratibu baina ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira - Tanzania Bara pamoja na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Tanzania - Zanzibar. Hivyo, utekelezaji wa mikataba hii hujumuisha watumishi wote wa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi zetu mbili zimekuwa zikishirikiana kwa pamoja kwenye vikao vya maamuzi vya mikataba hii. Pia pande zote mbili za Muungano zinanufaika na utekelezaji wa mikataba hii hususani kupitia, programu na miradi inayoratibiwa kupitia mikataba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendelea kusimamia utekelezaji wa mikataba ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa maslahi mapana ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kukabiliana na changamoto za kimazingira na athari za mabadiliko ya tabianchi, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maryam Azan.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninampongeza sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni haja ya kuwa na Mratibu Msaidizi kutoka Zanzibar ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa miradi hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha miradi ya mazingira inamalizwa kwa wakati ili iwanufaishe walengwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa Maryam kutoka Mkoa wa Kusini Pemba kwa kazi nzuri anayoifanya hasa kwenye suala la mazingira na athari kubwa ya mabadiliko ya tabianchi hasa katika Mkoa wa Kusini Pemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunafanya kazi zetu kwa kushirikiana, lakini Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - Zanzibar kwenye jambo la mazingira tunafanya kazi kwa kushirikiana. Sasa jambo la kutafuta mratibu ambaye atakuwa anasimamia haya mambo kwa sababu mambo mengi tumekuwa tunafanya kama taasisi, Wizara na Wizara, hatufanyi kama mratibu na mratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wazo lake na fikra yake aliyoipendekeza tunaichukua, tutakwenda kufanyia kazi kwa sababu hata wakati tunakwenda kusaini mikataba ya *adaptation fund,* hatukwenda kama mratibu na mratibu, tulikwenda kama taasisi na pande zote mbili tulishiriki. Tunakwenda kusaini mikataba ya *EBA,* tulikwenda kusaini mikataba ya miradi mbalimbali tulikwenda kama Wizara kutoka pande zote mbili. Lakini jambo la kutafuta mratibu atakayekuwa msaidizi tunalichukua na tunakwenda kulifanyia kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amsabi Mrimi nilikuona.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kutokana na mabadiliko ya tabianchi kumekuwa na mafuriko makubwa katika Mto Mara ambayo yamesababisha uharibifu wa mashamba katika Vijiji vya Nyiboko, Korenga, Nyasulumunti na Iselesele, Wilayani Serengeti, je, ni lini sasa Serikali itatekeleza mradi wake mkubwa uliopangwa wa kudhibiti mafuriko hayo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa aliwahi kuuliza swali hili na tuliona namna ambavyo tunaweza tukamsaidia na bahati nzuri tumeona athari kubwa ambayo inajitokeza huko na namna ambavyo wananchi wanaathirika kutokana na athari hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumemsikia na bado Serikali tunaendelea kutafuta fedha za kuona namna ambavyo tunaweza tukatengeneza mradi huu na kuweza kuwasaidia wananchi, ili wasiendelee kusumbuka na changamoto hiyo, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 582

**Hitaji la Mawasiliano ya Simu Kata za Bwakila Juu, Singisa na Mkulazi – Morogoro Vijijini**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza: -

Je, lini Kata za Bwakila Juu, Singisa pamoja na Mkulazi, Morogoro Vijijini zitapatiwa mawasiliano ya uhakika?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ilitoa ruzuku kwa watoa huduma za mawasiliano ya simu kwa ajili ya ujenzi wa minara mitatu katika Kata ya Mkulazi katika awamu tofauti. *Vodacom* ilijenga mnara katika Kijiji cha Mkulazi, Halotel - Kijiji cha Chanyumbu na *TTCL* - Kijiji cha Usungura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kwa upande wa Kata ya Bwakila Juu, *UCSAF* iliingia makubaliano na *TTCL* kwa ajili ya kupeleka huduma katika kata husika na utekelezaji unaendelea. Kwa upande wa Kata ya Singisa Kampuni ya *Airtel* itajenga minara mitatu kwa ajili ya kuhudumia Vijiji vya Nyamigadu '*A*', Nyamigadu '*B*', Lumba Juu, Lumba Chini, Ntala, Singisa na Kitengu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote itafanya tathmini ya hali ya mawasiliano ya simu katika maeneo husika baada ya kukamilika kwa utekelezaji wa miradi inayoendelea hivi sasa na kuchukua hatua stahiki endapo kutatokea na maeneo yatakayokuwa hayana mawasiliano ya kuridhisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa

Waziri, licha ya majibu mazuri nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya maswali mawili ya nyongeza ningependa kusisitiza katika Kata ya Bwakila Juu bado wana matatizo ya mawasiliano. Naomba sana muwasaidie kwa sababu hata barabara yao bado ni mbovu, mawasiliano ni mabovu na bado wanatumia milima kupata mitandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza, katika Manispaa ya Morogoro, Kata ya Magado, Mtaa wa *Fork Land* ambao mimi mwenyewe naishi, bado kuna matatizo ya mawasiliano, tungeliomba Mheshimiwa Waziri mtuongezee mnara wa Vodacom angalau wananchi waweze kupata mawasiliano kwa sababu ni wananchi wengi, lakini hawana mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, katika Kata ya Bunduki na Mgeta pia wana matatizo ya mawasilino, naomba sana muwaongezee minara kusudi waweze kupata mawasiliano mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa maswali yangu hayo.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyiongeza ya Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo aliyoyataja namna ya kushughulikia wakati mwingine siyo lazima kuongeza mnara, tunaweza tukaenda tukafanya ukaguzi na kama kutahitajika kuongeza mnara tutaongeza, lakini inawezekana tukahitajika kuongeza nguvu ya minara iliyopo.

Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuwaagiza *TCRA* Mkoa wa Morogoro waende leo kwenye eneo husika, wafanye tathmini na ndani ya siku tano walete matokeo ya tathmini hiyo, halafu

tutafanya uamuzi wa nini cha kufanya ili kuboresha huduma kwenye maeneo aliyoyataja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shamsia Mtamba, nimekuona.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za Tangazo na Naumbu, Kijiji cha Namgogori hakuna kabisa minara ya mawasiliano. Je, ni lini Serikali italeta minara ya mawasiliano katika Jimbo la Mtwara Vijijini kiujumla?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo aliyoyataja itabidi tukajiridhishe kama hayapo kwenye mradi wa minara unaoendelea sasa hivi wa *rural coverage,* tutafanya tathmini na tutaingiza kwenye mradi unaofuata ili wananchi wake wapate huduma za mawasiliano. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiswaga, nimekuona na Mheshimiwa Deo Mwanyika.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika minara zaidi ya 750 aliyoitoa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mimi katika Jimbo la Kalenga nilipewa minara kumi. Sasa ni lini mtakwenda kujenga minara hiyo katika Kata ya Msaka ambapo napo nilipewa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kiswaga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa minara 758 kwa ajili ya kupelekwa kwenye maeneo hasa ya vijijini na Jimbo la Mheshimiwa Kiswaga lilipata mgawo huo. Changamoto iliyotokea minara hii 758 haiwezi kuanza kujengwa yote kwa wakati mmoja, inajengwa kwa awamu na bila shaka Jimbo lake lipo katika mchakato huo wa ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, minara ambayo ilikuwa ijengwe na *Vodacom* kulikuwa na changamoto waliagiza vifaa vyote kwa wakati mmoja, kwa hiyo, vilichelewa kidogo kufika, lakini hivi tunavyoongea vifaa vyote vinavyotakiwa vipo nchini na ndani ya muda mfupi tutaona hiyo minara ikiinuka na wananchi wake watapata huduma wanazostahili kupata. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mnazungumza kwa sauti kubwa, naomba mzungumze taratibu ili tuwe tunaelewana.

Mheshimiwa Deo Mwanyika, halafu Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa namna ambavyo anafanya kazi na namna ambavyo Wizara inabadilisha nchi yetu kidigitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikuliza swali kuhusiana na mnara mmoja tu, wengine wanaongelea minara 10 au 15 mimi ninara miwili tu ambao ni mnara wa Kijiji cha Uliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi niliambiwa ungejengwa mwaka jana, mwaka jana nikaambiwa utaingizwa kwenye bajeti ya mwaka huu, lakini hata kwenye bajeti ya mwaka huu mimi sijaona, nimeona mnara mwingine wa kijiji kingine, lakini Uliwa ndipo kwenye tatizo hasa la mawasiliano na pana shule,

sekondari, zahanati, kituo cha afya, lakini hawana mawasiliano, wapo chini. Mheshimiwa Waziri ni lini sasa Uliwa itaingizwa kwenye bajeti na itapata mnara huu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Mwanyika, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru kwa pongezi zake kwa niaba za watumishi wa Wizara tunazipokea ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Deo amekuwa akilifuatilia jambo hili siyo mara moja au mbili, nataka nitoe ahadi ndani ya Bunge lako mimi na Mheshimiwa Deo tutakaa pamoja tulishughulikie hili jambo tuhakikishe tunalimaliza. Mheshimiwa Deo nikimaliza nitakuja tukae, nichukue taarifa zako, nione wapi tunakwama, lakini nikuhakikishie kwamba nia ya Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Samia ni kuhakikisha kila Mtanzania popote alipo anaunganiushwa na huduma za mawasiliano. *(Makofi)*

**MWNEYEKITI:** Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Mheshimiwa Waziri natambua mikakati inayoendelea ya kuunganisha Mkoa wa Rukwa na Katavi kwenye maeneo ambayo hayana mawasiliano na kwa sababu mawasiliano ni haki ya wananchi wote, ningependa kufahamu, kuna kata nne ambazo bado hazina mawasiliano. Kata za Mkinga, Kipili, Isale na Mkwamba, ni lini watu hao watapata mawasiliano?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mikakati inayoendelea lengo lake ni kuhakikisha kila Mtanzania popote alipo anapata huduma za mawasiliano na hasa mikoa ya pembezoni. Mimi nimefanya ziara kwenye baadhi ya maeneo ya Rukwa, Sumbawanga, Katavi na kadhalika na ninajua changamoto iliyopo na hasa maeneo haya ya mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kata alizozitaja nitakwenda kuangalia kwenye Mradi wa Tanzania ya Kidigitali kama hazimo jambo ambalo siamini, kama hazimo nitahakikisha zinaingia kwenye mradi unaofuata na kama zimo tutasukuma ili mradi huo uanze mapema tuwahudumie wananchi wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Nape Moses Nnauye kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, aulize swali lake.

Na. 583

**Kuanzisha Mamlaka ya Maji Mkoa wa Pwani**

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE K.n.y. MHE. SILYVESTRY F. KOKA** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kuanzisha Mamlaka ya Maji Mkoa wa Pwani ili kuondoa changamoto ya maji maeneo mengi ya mkoa huo?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya huduma majisafi na salama katika Mkoa wa Pwani ni wastani wa 79.8% kwa vijijini na 90% kwa mijini ambapo huduma hiyo inatolewa kupitia Wakala wa Maji na

Usafi wa Mazingira Vijijini *(RUWASA)* kwa upande wa vijijini na kwa maeneo ya mijini huduma hiyo inatolewa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam *(DAWASA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inaridhishwa na taasisi zinazotoa huduma ya majisafi na salama katika Mkoa wa Pwani ambapo maeneo yote ya mijini yanapata huduma za maji safi kwa viwango mbalimbali. Hata hivyo, Serikali ipo tayari kufanya mabadiliko yoyote yanayolenga kuboresha eneo la utoaji huduma ya maji katika Mkoa wa Pwani pindi itakapoonekana inafaa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka, tunashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zimeendelea kuwepo Mkoa wa Pwani kwenye suala la maji, je, lini Serikali itaanza kujenga Mradi wa Maji uliopo Pangani ukizingatia toka mwaka jana mwishoni tulisaini mkataba? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Serikali ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa miradi ya maji nchini kote. Vilevile kwa upande wa Mradi huu wa Pangani, Serikali tayari ipo katika hatua nzauri kabisa za kuendelea na utekelezaji wa mradi huu. Nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge atupatie nafasi Serikali ili tuhakikishe kwamba mradi huu unakamilika na wananchi wa Pwani na maeneo maeneo yote yanayozunguka mradi huo wapate huduma ya maji safi na salama, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, aulize swali lake.

Na. 584

**Hitaji la Chuo cha Ufundi *VETA* – Ifakara**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Chuo cha Ufundi *VETA* katika Mji wa Ifakara?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa sasa inaendelea na utekelezaji wa azma ya kujenga Chuo cha Ufundi Stadi katika kila mkoa na wilaya nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi katika wilaya 64 ambazo zilikuwa hazijajengewa Vyuo vya Ufundi Stadi pamoja na Chuo cha Mkoa wa Songwe. Aidha, Wilaya ya Kilombero ni miongoni mwa wilaya 64 ambazo zinajengewa vyuo vya ufundi stadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali imeshapeeka kiasi cha shilingi 324,694,243 pamoja na vifaa vya ujenzi ikiwemo nondo na simenti kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Kilombero ambacho kitatoa mafunzo kwa vijana wa Wilaya ya Kilombero ikiwemo Mji wa Ifakara. Aidha, ujenzi wa chuo hiki upo katika hatua ya ujenzi wa kuta za boma na ufungaji wa linta pamoja na ukamilishaji wa misingi, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza nishukuru Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kweli inatusaidia sana. Tuliomba Chuo cha *VETA* Wilaya ya Kilombero tumepewa, tuliomba barabara ya lami tumepewa, Kiwanda cha Sukari shilingi bilioni 500 tumepewa, mradi wa maji shilingi bilioni 43 tumepewa, Hospitali ya Halmashauri tumepewa, kadhalika na kadhalika. Kwa kweli watu wanaochafua huko nje waache tunamshukuru sana Dkt. Samia kwa kazi kubwa anayoifanya. Naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, halmashauri ambazo zipo katika wilaya hazikupata Vyuo vya *VETA*, tulikubaliana kwamba, ziatapata shule maalum za ufundi. Je, ni lini ujenzi utaanza wa Shule Maalum ya Ufundi katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Ifakara kuna Chuo cha Ufundi vile vya *FDC* ambavyo vina eneo kati kati ya Mji wa Ifakara na eneo lile limekuwa likipata wavamizi mara kwa mara, je, Serikali haioni umuhimu wa kwenda kuzungushia *fence* katika chuo hicho ili kulinda eneo la chuo hicho? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kupekee tupokee pongezi hizo za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, yeye ndio amewezesha hayo yote kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza kwa kupande wa shule zile za ufundi nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge ni kweli Serikali ina azma ya kujenga shule za ufundi katika majimbo yale ambayo hayakujengewa Vyuo vya *VETA*. Tunafahamu kwamba hivi Vyuo vya *VETA* vinajengwa katika wilaya pia

tunafahamu kuwa zipo wilaya ambazo zina majimbo zaidi ya moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, iwapo kama *VETA* imejengwa katika Jimbo moja na wilaya hiyo ina majimbo zaidi ya moja, tafsiri yake shule hizi za ufundi tunakwenda kujenga kwenye yale majimbo ambayo yamekosa fursa za kujengewa vile Vyuo vya *VETA*.

Kwa hiyo, nikuondoe wasiwasi hivi sasa tupo katika maandalizi ya fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule hizi zipo tayari. Tunafanya upembeuzi yakinifu pamoja na kufanya zile *site visit* kwa ajili ya kukagua yale maeneo ambayo zitajengwa shule hizi za ufundi na tunapofika Julai tunatarajia shule hizi ziweze kuanza kujengwa rasmi. Kwa hiyo, lini tunaanza? Tutaanza mwaka ujao wa fedha kwa maana Julai mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa pili kwenye vyuo vyetu vile vya *FDC*, ni kweli tuna vyuo vya *FDC* karibu 54 katika nchi yetu. Vilikuwa kwenye hali mbaya sana, vyuo hivi Serikali imeshafanya ukarabati, tumeongeza majengo kwenye baadhi ya maeneo ambako kulikuwa hakuna majengo, tumefanya ukarabati kwenye yale majengo ya zamani, tumenunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwenye vyuo hivi, kwa vile sasa shughuli hizi zote zilikuwa zinakwenda kwa awamu, awamu inayofuata sasa tunaangalia kwenye yale maeneo ambayo kuna uhitaji wa kujengewa uzio kwa ajili ya kujenga uzio.

Kwa hiyo, nikuondoe wasiwasi, tunaenda kwa awamu na uzio kwenye vile vyuo ambavyo viko mijini ambavyo tunaona kabisa kuna haja ya kujenga uzio tutakwenda kujenga uzio, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maganga nimekuona, Mheshimiwa Zuena Bushiri atafuata.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri, kwanza ninakushukuru kwa kunipa Chuo cha *VETA* Mbogwe, lakini kazi haifanyiki mpaka sasa hivi hata mafundi wametoka *site*. Mheshimiwa Waziri, shida ni nini? Kwa sababu wananchi walijua kwamba mwaka kesho tutaenda kuanza kukitumia hicho chuo. Ninahitaji majibu yako ili kusudi wananchi wa Mbogwe wajue, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Maganga, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa vyuo hivi 64 vya wilaya pamoja na kile kimoja cha mkoa tunajenga kwa awamu na nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, baada ya kumaliza misingi kuna vifaa ambavyo inabidi tuagize. Tumefanya *bulk purchase* kutoka viwandani moja kwa moja. Katika zile karakana na majengo yale makubwa yote tunatumia Mfumo wa *LGS (Light Gauge Steel),* zile ni *fabricated metals* ambazo zinatoka kiwandani moja kwa moja. Kwa hiyo, unapoona ujenzi umesimama tayari tumesha-*press order* kwa ajili ya hizo *fabricated metals* na baada ya muda si mrefu zitakuja na zikishafika pale *site* ni kazi ya mwezi mmoja tu majengo yale yote yatakuwa tayari yameshanyanyuka.

Kwa hiyo, nikuondoe wasiwasi, kazi hiyo inaendelea, fedha zimeshalipwa kule *ALAF* na shughuli inaendelea kwa sababu zinakuwa *imported*. Mara baada ya kufika tutakuja hapo Mbogwe na kukamilisha hiyo kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuena Bushiri, Mheshimiwa Kakoso nimekuona.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Moshi ina vijana wengi sana ambao wanahitaji elimu ya ufundi. Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha *VETA* katika halmashauri hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimwia Mwenyekiti, ninaomba nijibu swali dogo la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwisha kujibu kwenye maswali ya msingi kwamba kwa sasa baada ya kukamilisha ujenzi wa vile vyuo 25 vya awamu ya kwanza katika wilaya 25 na hivi 64, tutakuwa hatuna wilaya ambayo haina Chuo cha *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba kunawezekana kukawa na umbali wa namna moja au nyingine lakini ninaamini pale Moshi tuna Chuo cha *VETA* ambacho kiko pale Moshi, ni chuo cha mkoa, lakini vilevile kina-*save* kama chuo cha wilaya, lakini kwenye zile wilaya nyingine za pembezoni, ukienda Rombo, ukienda Hai, ukienda Siha, kote kule tumejenga Vyuo vya *VETA* na yale majimbo ambayo hayana vyuo tunakwenda kujenga shule za ufundi ku-*complement* pale ambapo Chuo cha *VETA* kimekosekana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtaturu nilikutaja. Mheshimiwa Kakoso halafu Mheshimiwa Mtaturu.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ni miongoni mwa wilaya ambazo zimeanza ujenzi wa *VETA* eneo la Wilaya ya Tanganyika, lakini kwa bahati mbaya sana mpaka sasa tunavyozungumza ujenzi umekwama takribani zaidi ya miezi mitano. Ni lini Serikali itapeleka fedha kukamilisha ujenzi wa *VETA* Wilaya ya Tanganyika?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Kakoso, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali tumeshapeleka fedha na ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, pesa tulizopeleka hizi shilingi milioni 324.6 katika kila *site*, hizi zimekwenda kwa ajili ya zile *local materials*, kwa maana ya mchanga, kokoto, mawe, maji, lakini pamoja na gharama za kulipa mafundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zile *materials* nyingine zote Wizara inanunua kwa mfumo wa *bulk purchase* kwa maana ya simenti, nondo, mabati pamoja na zile *LGS (Light Gauge Steel)* kwa ujumla wake. Kwa hiyo, iwapo kama misingi yote imeshakamilika na maboma yameshanyanyuliwa, tafsiri yake kinachosubiriwa sasa ni vile vifaa kutoka kiwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Kakoso, hivi sasa tayari vifaa hivi vimeshaagizwa na mara baada ya kufika tutavipeleka katika kila *centre* kuhakikisha kwamba majengo hayo yananyanyuka. Lengo letu ifikapo mwezi wa 10 vyuo hivi kwa awamu hii ya kwanza yale majengo tisa yawe yamekamilika ili mwezi wa 11 tuweze kuanza kutoa mafunzo rasmi, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtaturu na Mheshimiwa Zacharia Issaay niliwaona.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nianze kwa kumshukuru sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia fedha shilingi 2,400,000,000 kujenga chuo bora kabisa cha *VETA* Wilaya ya Ikungi. Sasa hivi tunavyoongea chuo kimeanza kazi chini ya Mkuu wa Chuo Ndugu Mathias Luhanga na wanafunzi wako darasani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niombe tu Mheshimiwa Waziri kwamba kwa ajili ya mambo ya kiutawala chuo chetu

kinahitaji usafiri. Ninaomba sana kujua ni lini Serikali itawaletea gari kwa ajili ya kufanya kazi za kiutawala katika Chuo chetu cha *VETA* Ikungi? Ahsante sana *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nikijibu swali dogo la Mheshimiwa Mtaturu, Mbunge wa Ikungi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwenye vyuo vyetu 25 tuna changamoto ya usafiri lakini nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, safari ni hatua na hatua tumeshaanza, kimsingi kwanza tulianza kujenga yale majengo, lakini baadaye tukajaribu kutafuta watumishi kwa ajili ya mafunzo hayo kuanza na hivi sasa mafunzo yameanza. Tumeanza kupeleka vifaa na hatua inayofuata ni kupeleka sasa vile vyombo saidizi kwa ajili ya kuhakikisha wataalamu wetu, walimu wetu na watumishi wetu wanafanya kazi zao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi, katika bajeti yetu ijayo tumeweka fungu kwa ajili ya ununuzi wa magari, kwa ajili ya vyuo hivi vya *VETA*, *FDC* pamoja na vyuo vyetu vya ualimu. Tunaamini katika utekelezaji wa bajeti ya mwakani mambo hayo yatakwenda kufanyika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia, Mheshimiwa Dkt. Kyombo nimekuona.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, tunaishukuru Serikali kwa ukarabati mkubwa uliofanywa katika Chuo *Tango FDC*, Mbulu Mjini, je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kumalizia yale majengo yaliyobaki kukarabatiwa ili chuo kile kiwe na hadhi?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nikijibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Zacharia, Mbunge wa Mbulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli pale Tango tumefanya ukarabati mkubwa na baadhi ya majengo bado hatujakamilisha. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Zacharia, lakini ninakumbuka juzi ulikuja kwenye meza yangu tukalizungumza jambo hili pamoja na suala la kwenda kule Tango na nikakuahidi kwamba tusubiri tukamilishe shughuli za Bunge ili tuweze kwenda kuona hali halisi ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikuondoe wasiwasi, katika Mradi wetu wa *EP4R* ambao tunataraji kuanza mwaka ujao wa fedha, tuna mpango wa kukarabati majengo yote katika vyuo vyote vya *FDC* ambavyo bado hatujafanya ukarabati. Kwa hiyo, kama nilivyokwisha kujibu kwenye swali moja la nyongeza hapa la *FDC* kule Ifakara, basi vilevile na Tango tutakwenda kufanya kama tutakavyofanya Ifakara. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kyombo, atafuatia Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi na ninaipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan chini ya Wizara ya Elimu, Waziri na Naibu Waziri kwa kuanza ujenzi wa Chuo cha *VETA* ndani ya Wilaya ya Missenyi. Chuo hicho ni matarajio makubwa ya Wana-Missenyi na kimeanza lakini spidi yake kwa kweli hairidhishi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini sasa tutapata vifaa vya ujenzi ili tuweze kwenda kwa *speed* na tuweze kupata chuo hicho ambacho ni matarajio makubwa kwa Wana-Missenyi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali dogo la

nyongeza la Mheshimiwa Kyombo, Mbunge wa Missenyi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwisha kujibu kwenye maswali mengine ikiwemo na hili la Mheshimiwa Kyombo kule Missenyi, sasa hivi tunachosubiri ni vile vifaa ambavyo ni *imported materials*, zile *fabricated metals (LGS)* kwa ajili ya majengo yetu yale makubwa, makarakana yale manne yote yale yanahitaji *materials* hizo, lakini pamoja na bati ambapo nimesema tayari tumesha-*press order,* tumeshalipa na vifaa hivyo viko njiani kuja. Mara vitakapofika mtashangaa ile *speed* yetu tutakayokwenda kule, ndani ya mwezi mmoja yale majengo yote na mazingira ya pale yatakuwa yamebadilika kabisa na tunaamini mpaka itakapofika mwezi wa 10, Missenyi tutakuwa tumekamilisha yale majengo makubwa na huduma pale zinaweza kuanza mara moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo, Mheshimiwa Dkt. Mnzava nimekuona.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Mheshimiwa Waziri, kwanza niipongeze Serikali kwa ujenzi wa *VETA* nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, kutokana na kwamba dunia ya sasa mabadiliko ya teknolojia, maeneo mengi ya *VETA* ambazo zinajengwa, masomo yanayotolewa ni ya aina ile ile, ufundi ujenzi nyumba, ufundi cherehani na ufundi Seremala lakini soko la vijana nje linahitaji masomo mengine. Ufundi bomba, ufundi umeme wa magari, ufundi umeme wa majumba, lakini mitambo ya gesi kama usambazaji wa gesi unaoendelea nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni upi mkakati wa Wizara, wakati Mheshimiwa Rais anaendelea kujenga *VETA* nchini, ni upi mkakati wa Wizara kubadilisha *syllabus* ziendane na soko la sasa ili tuokoe vijana wengi wa Kitanzania wapate fursa hiyo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la Mheshimiwa Sanga kama ifuatavyo, Mheshimiwa Sanga anatoa ushauri kwa maana ya kubadilisha mtaala, lakini nikuondoe wasiwasi Mheshimiwa Sanga tayari Mheshimiwa Rais alishaliona hilo na alishaagiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza na maboresho makubwa ya mitaala yetu kuanzia shule za msingi, sekondari mpaka vyuo vikuu, lakini Mheshimiwa Rais aliagizwa kwamba, *VETA* hizi zinazojengwa, basi mitaala yake na masomo yake na kozi zake ziendane na shughuli za kiuchumi za sehemu husika, kwa maana tunakwenda kufanya *customization* katika vyuo hivi kwa lengo la kuhakikisha kwamba zile shughuli za kiuchumi zinazofanyika katika maeneo hayo ziweze kufundishwa katika vyuo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yale maeneo ambayo tunachimba madini tutakuwa na kozi za madini zinafundishwa kwenye vyuo hivi, yale maeneo ambayo tunashughulika na masuala ya uvuvi kutakuwa na kozi za uvuvi zinafundishwa kwenye maeneo haya, kule kwangu nako kimejengwa chuo kama hiki, kuna masuala ya utalii, lakini vilevile masuala ya *hospitality* yatafundishwa kwenye vyuo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunakwenda kuhakikisha zile shughuli sasa za kiuchumi ndizo zitakazofundishwa, tukiongezea na hizi kozi nyingine za *general* ambazo kila mmoja wetu anapaswa kuzifahamu ili hata bomba likikatika pale nyumbani kwako huna haja ya kutafyta fundi, wewe mwenyewe unaweza kurekebisha kwa namna moja au nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huo ndiyo mpango wa Serikali. Mheshimiwa Rais ameshatoa agizo na sisi kama Wizara ni lazima tutekeleze kwa kadri maagizo yalivyotolewa.

**MWENYEKITI:** Nimemtaja Mheshimiwa Dkt. Mnzava, Mheshimiwa Dkt. Kimei nilikuona. Tunamalizia na Mheshimiwa Yahya.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Chuo cha *VETA* kilichopo Manispaa ya Shinyanga ni chuo kongwe na kinahitaji ukarabati wa miundombinu. Ni upi mpango wa Serikali kukarabati Chuo cha *VETA* Manispaa ya Shinyanga? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nikijibu swali dogo la Mheshimiwa Dkt. Mnzava, ni kweli tuna vyuo vyetu, baadhi ya vyuo vyetu vya mikoa ni vya muda mrefu, majengo yake ni chakavu na miundombinu mingine ni chakavu, hata vifaa vilivyokuwa vinatumika ni vile vya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Dkt. Mnzava, tuna miradi mbalimbali ambayo tumeshafanya maandiko yake na maandiko hayo yatakapokamilika na miradi hii kuanza tutakwenda kufanya ukarabati kwenye vyuo vyetu vyote kongwe kikiwemo na hiki Chuo cha Mkoa wa Shinyanga. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba katika Kata ya Mwika Kaskazini kwenye Jimbo langu la Vunjo kwenye Shule ya Msingi ya Lole kuna Chuo cha *VETA* ambacho kimetelekezwa kutoka mwaka 2000. Majengo yamechakaa, lakini kuna baadhi ya *tools* za kutumia kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kinachohitajika pale ni kukarabati yale majengo na kupata walimu wa kufundisha, basi pamoja na kuongeza hasa hivyo vifaa vya kufundishia. Je, ni lini Serikali itachukua hatua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sijui ni mara yangu ya tatu ninauliza swali hili, lakini nimeona nirudie kwa sababu wale wananchi wanateseka sana. Jimbo la Vunjo liko pacha na Jimbo la Moshi Vijijini kwenye halmashauri moja. Kwa hiyo, kuna

*disadvantages* nyingi sana ambazo tunapata kwenye ku-*allocate* hizi *facilities*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nikijibu swali dogo la Mheshimiwa Dkt. Kimei ni kuwa jambo hili ulilolizungumza ninaomba tu tutoe maagizo kwa Mkurugenzi wetu wa *VETA*, kwanza kwenda kuona hilo eneo, lakini Mheshimiwa Dkt. Kimei kama utaridhia ninadhani ni muhimu na sisi tukaenda tukaona, wazungu wanasema; *"the seeing is believing." (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninadhani kuna umuhimu wa kupanga ratiba na sisi wenyewe kama Wizara, mimi binafsi niende nikaone tuweze kufanya tathmini ya kina ili tuweze kujua kitu gani, *measures* zipi tuweze kuchukua ili kama ni chuo ambacho kimeshakabidhiwa kwenye Wizara, basi tufanye ukarabati kama ulivyoshauri. Tupeleke vifaa pamoja na walimu ili mafunzo hapo yaanze kutolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia tunaomba tumwagize Mkurugenzi wa *VETA* aweze kwenda eneo hilo kwa haraka na sisi tukimaliza Bunge hapa tutakwenda. Mheshimiwa Dkt. Kimei tutapanga na nitakuja hapo kwako tupange ratiba ya kwenda huko haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunamalizia Mheshimiwa Yahaya Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Wilaya ya Manyoni ina majimbo mawili. *VETA* inayoendelea kujengwa katika Manyoni iko katika Jimbo la Manyoni Mashariki. Unawaambiaje watu wa jimbo langu eneo la Itigi kuhusu ujenzi wa shule ambayo mmeitaja? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nikijibu swali dogo la

Mheshimiwa Massare ni kwamba Mheshimiwa Massare anajua na tulishazungumza suala hili na alikuja ofisini na akaangalia orodha ya shule zitakazokwenda kujengwa za ufundi na Wilaya ya Manyoni, ilikuwa Manyoni imekosewa, Manyoni Kaskazini na Manyoni Kusini tukarekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Massare, shule yake ya Ufundi ipo, tumeshafanya marekebisho mwanzoni kulikuwa na *typing error*. Shule ile itakwenda kujengwa katika jimbo lake kama vile alivyoshauri yeye mwenyewe na kazi hii itaanza Julai mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mengi sana ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 585

**Kampuni Zilizoshiriki Ununuzi wa Kahawa – Kagera**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza: -

Je, kampuni gani zilishiriki ununuzi wa kahawa Mkoani Kagera kwa mwaka 2023?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, katika msimu wa masoko ya kahawa wa 2023/2024, jumla ya kampuni 23 na Vyama vya Ushirika vitatu vilishiriki kwenye ununuzi wa kahawa ya maganda *(dry cherry)* na kahawa maalum *(certified coffee)* katika Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanunuzi wa kahawa ya maganda *(dry cherry)* walikuwa ni *Tanin Global Limited, Blue Effort, Nkuban International Company Limited*, *Amri Amir Al-Habssy, Karagwe Estate Limited, Source of the Nile Commodities Limited, Kyejus Coffee Company Limited, KCU Limited, Kongeru Tanzania Limited, Ubumwe Crops Company Limited, Zuraja Trading Company Limited, Tanzania Quality Coffee Limited, J.K Supplies and Consultancy Company, Megnacio Company, OTM Trading Company Limited, Mweru and J Coffee, Shayakye Trading Company Limited, Izigo Coffee Limited, Jocta International, Azania Fresh Food Industry Limited, Johansen Company Limited* na *Atadals Group Limited.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni zilizoshiriki ununuzi wa kahawa maalumu *(certified coffee)* ni *Kaderes Peasants Development Plc, Karagwe Estate Limited, KCU Limited*, pamoja na Vyama vya Ushirika vya Juhudi *AMCOS*, *Nkwenda AMCOS* na *Mkombozi AMCOS*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, ninataka kujua mkakati wa Serikali wa kuzisaidia *AMCOS,* badala ya kuuza kahawa ghafi *(dry cherry)* wakauza *fine coffee* ambayo inaitwa *FAQ*. Sababu ni kwamba *FAQ* bei ya *dry cherry* ni ndogo ukilinganisha na *FAQ*. Kama hii inauzwa shilingi 5,000 kama mnada ulivyo leo, *FAQ* inauzwa shilingi 10,000 kwenye masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuuza *FAQ* wataweza kupata faida ya mbolea ambayo wanakuwa wanainunua baada ya kuuza hizo kahawa ambayo ni maganda. Ninataka kujua mkakati wa Serikali wa kuzisaidia hizo *AMCOS* ili ziweze kuuza *FAQ* kwa faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kampuni ambazo zimekuwa zikinunua *specialized coffee* wakati mwingine huenda moja kwa moja kwenye *AMCOS* na hununua bei ndogo ukilinganisha na bei ya minada. Ni nini kauli ya Serikali kuzitaka zile

kampuni kununua bei sawa na mnada tofauti na ilivyo leo au zaidi ya hapo? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, jambo la kwanza tu nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi Serikali moja ya mikakati yetu ni kuhakikisha kwamba tunazi-*empower* hizi *AMCOS*. moja kwa ku-*invite* wawekezaji wengi kuja kutengeneza viwanda hapa nchini ambapo watakuwa na nafasi ya kuongeza thamani ya kahawa na kuuza kwa bei nafuu. Kwa hiyo, hilo jambo tunalo na tunalifanyia kazi na tumeunda Tume maalumu kwa ajili ya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bei ndogo inayonunuliwa katika hizo *AMCOS* katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja kwenye hivi vyama, kauli ya Serikali ni kwamba sasa hivi tumetangaza matumizi ya mnada wa *TMX* na tumewataka Vyama vya *AMCOS* vitumie ule mnada ili kupata bei ambayo inaridhisha. Haturuhusu sana watu kwenda kununua moja kwa moja kwa mkulima kwa sababu wamekuwa wakiwanyonya.

Kwa hiyo, huo ndio msimamo wa Serikali na tutaendelea kusimamia. Kwa hiyo, kikubwa hapa kwa taarifa uliyotoa, sisi tutaendelea kufuatilia ili jambo hili lisiendelee, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Lugangira, nimekuona Mheshimiwa Nyamoga na Mheshimiwa Profesa Ndakidemi; Maswali mafupi.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kufahamu ni nini mkakati wa Serikali kuweka utaratibu wa kuuza vanila, hususani mkoani Kagera? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, mkakati wa Serikali wa sasa ni kwamba zao la vanila tumeliingiza kati mnada wa *TMX* kwa maana linauzwa kwa mnada na kwa mfano tulikuwa kule Kyela pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu, tulienda kuzindua msimu wa ununuzi wa vanila kupitia mfumo wa *TMX*. Kwa hiyo, mfumo ule siyo tu utatumika Kyela ni kwamba utatumika katika maeneo yote wanayozalisha mazao ya vanila ikiwemo Kagera, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nyamoga nilikuona, tunamalizia na Mheshimiwa Dkt. Abbas.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, katika Kata ya Ukwega yaani Vijiji vya Mkalanga, Makungu, Lulindi na Ukwega yenyewe kuna kilimo cha kahawa, lakini wanakatishwa tamaa na ukosefu wa soko, kwa hiyo zao lile linaelekea kuondoka katika eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ipo tayari kupeleka wataalamu na kuangalia njia bora ya kwanza kukiimarisha kilimo kile, lakini pili kupata soko ili waendelee na kilimo cha kahawa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Nyamoga kwamba Serikali tupo tayari, moja tutaleta wataalamu na hili lipo ndani ya uwezo wetu, lakini pili tutaendelea kutafuta masoko, lakini soko kubwa sasa hivi tunatumia mnada, lakini vilevile tunazungumza na balozi zetu kuleta wawekezaji zaidi kwa ajili ya kutengeneza viwanda ndani vya kuongeza thamani ya zao ambayo ndiyo yatakuwa moja ya sehemu ya masoko makuu ya kahawa ambayo inazalishwa nchini, kwa hiyo, hilo lipo na tunaliweza, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali kama Serikali ina mikakati gani mahususi ya kutafuta wanunuzi na masoko yenye tija kwa wakulima wa kahawa Tanzania?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimjibu tu Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, Mbunge wa Jimbo la Moshi Vijijini kwamba moja ya mkakati wetu mkubwa, kwanza ilikuwa ni kumuondoa mkulima wa kahawa katika ule utaratibu wa uuzaji wa kahawa wa zamani, ambapo sasa hivi zao la kahawa linauzwa kwa kupitia njia ya *TMX* kwa maana mnada ambapo wanunuzi wanakutana pamoja na ku-*bid price* na yule ambaye ana-*tender* kwa bei ya juu ndiyo anayepewa nafasi ya kununua zile kahawa, kwa hiyo, huu ni mkakati wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wetu wa pili sasa hivi tumeshazungumza na balozi zote nchini ambazo wamekuwa na jitihada kubwa ya kutafuta masoko ya kahawa yetu kule nje ya nchi ambako ndiyo wamekuwa watumiaji wakubwa, hii naamini kwamba itasaidia kuongeza bei ya zao la kahawa na tumekuwa tukifanya hivyo na mabalozi wamekuwa wakitupa mrejesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kuna *promising future* kwenye zao la kahawa, kwa hiyo tuwatake wakulima wote waendelee kuzalisha kahawa kwa wingi na sisi kama Serikali kupitia taasisi zetu za *TARI* tutaendelea kutoa mbegu bure za kahawa ili kulifanya zao hili liendelee kuleta fedha nyingi sana za kigeni hapa nchini, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abbas na Mheshimiwa Mulugo.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, watu wasishangae kumwona Mbunge wa Kinondoni anaulizia swali la kahawa, hatulimi kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa mujibu wa Jarida la *Coffee Review*, Tanzania ni nchi ya nne kwa uzalishaji wa kahawa Afrika na ni nchi ya 14 duniani, tuna sifa nzuri, lakini ukienda

kwenye maduka ya unywaji kahawa huko Europe na sehemu nyingine huikuti kahawa ya Tanzania ikitangazwa kama ilivyo kahawa ya Colombia, Brazil, Kenya na Uganda. Ni nini kauli ya Serikali katika kuifanya kahawa yetu ya Tanzania itangazwe na isifike duniani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimpongeze vilevile Mbunge wa Kinondoni kwa kuuliza swali hili la kimataifa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kikubwa tu nimthibitishie Wizara ya Kilimo tukishirikiana na watu wa Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia taasisi zao hususani *TanTrade* wamekuwa wakienda katika yale masoko makubwa kutangaza bidhaa hizi, lakini vilevile kupitia balozi zetu na miongoni mwa zawadi kubwa ambazo tumekuwa tukizitoa kwa marafiki zetu zile nchi ambazo tumekuwa tukitembelea ni pamoja na kupeleka bidhaa za kilimo hususani kahawa na korosho katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile yote tu ni sehemu ya moja ya kutangaza, kwa hiyo tu niseme kwamba tutaongeza mkazo na msisitizo pamoja na bajeti ili kuhakikisha sasa kahawa ya Tanzania iwe inanyweka katika maeneo mengi hapa nchini, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mulugo.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetokea hivi karibuni kule Songwe baadhi ya kampuni zinakuja kununua ufuta kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani kwa Mfumo wa *TMX*, lakini wametokea matapeli baadhi ya kampuni wanataja bei kubwa na *AMCOS* na wakulima wanakubali wanauza ufuta kwa kutumia njia ya minada safi. Baada ya siku mbili au tatu kadiri ya sheria hawalipi fedha na wanapotea na wakulima wanabaki wanahangaika. Nini kauli ya

Serikali ya kudhibiti makampuni haya kwa nini wasiwa-*blacklist* au kuwafungia kabisa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, anachokizungumza Mheshimiwa Mulugo ni jambo ambalo sisi kama Wizara ameshatufikishia na kama Wizara tupo katika hatua za kulifanyia kazi, lakini kitu cha kwanza ambacho nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge, sasa hivi kama Wizara tutafanya *due diligence* kwenye kwa maana uhakiki kabla ya zile kampuni kwenda kununua, ama ku-*bid* kwa wakulima kwa sababu mtu anapo-*bid* bei ya juu na akishindwa kuwalipa wakulima maana yake anawarudisha nyuma wakulima katika maeneo husika.

Kwa hiyo, jambo hili lipo na tutalitolea taarifa yake kamili kwa sababu lipo katika mchakato wa kuhakikisha kwamba tunadhibiti hizi changamoto ambazo zimejitokeza, ahsante. *(Makofi)*

**MWNYEKITI:** Mheshimiwa Benardeta Mushashu, nilikuona.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Kwanza kabisa naipongeza Serikali na hasa nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuzindua huo mpango wa kununua vanila kwa njia ya mnada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa palikuwa hakuna soko la uhakika kwa ajili ya ununuzi wa vanila, mkoani Kagera wakulima wamelizwa mwaka jana kuna mtu amejitokeza amechukua vanila zote, lakini hakumlipa mkulima hata mmoja. Je, Serikali mna mpango gani kuwasaidia hao wakulima wa vanila Mkoa wa Kagera waweze kulipwa hizo hela ambazo walidhulumiwa tangu mwaka jana? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ni kwamba moja ya hatua ambayo tutachukua ni kwamba huyo mnunuzi ambaye alinunua vanila na hakuwalipa wananchi maana yake sisi kama Wizara tutamwita na ikibidi tutachukua hatua za kisheria, lakini jukumu letu kama Serikali ni kuhakikisha fedha yoyote ya mkulima inalipwa na hilo sisi tutalifanya. Kwa hiyo nimwondoe tu shaka Mheshimiwa Mbunge na wakulima wa Kagera kwamba jambo hilo limetufikia na tunalifanyia kazi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana, nakushukuru sana kwa majibu ya maswali mengi ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa.

Na. 586

**Ujenzi wa Chuo cha Afya – Vwawa**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Chuo cha Afya Vwawa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Chuo cha Afya Vwawa utaanza mwezi Oktoba, 2024 na Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 2.9 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kupitia fedha za Mradi wa Mama na Mtoto, kwa ajili ya kujenga jengo la mafunzo mseto *(academic complex)*. Aidha, tayari utaratibu wa kupata

eneo umefanyika na kiasi cha shilingi milioni 151 kimetumika kwa ajili ya kulipa fidia ya ardhi kwa wananchi waliopisha eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhet Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naishukuru Serikali kwa majibu hayo mazuri ambayo imeyatoa, lakini ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha 2023/2024 fedha hizi zilikuwa zimetengwa, hasa ningependa kujua nini kimetokea chuo hicho kimeshindwa kuanza kujengwa kwa mwaka huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, ni aina gani ya mafunzo na katika ngazi gani chuo hiki tarajiwa kinategemea kuyatoa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Hasunga kwa kuwa mfuatiliaji mzuri wa ujenzi wa Chuo cha Afya Vwawa, lakini kubwa maswali yake mawili pia la kwanza, kipi kimetokea fedha zilizotengwa 2023/2024 hazijafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni kuchelewa kwa kulipwa kwa fidia na hivyo tumeshindwa kuanza ujenzi kwa sababu fidia ilichelewa kulipwa, lakini jambo la pili Mheshimiwa Hasunga ni kwa sababu bado chuo hakijapata hatimiliki na hili nikuombe sana Mheshimiwa Hasunga ukatusaidie pamoja na mamlaka nyingine za Serikali mkoani Songwe na hususani Vwawa kuweza kupata hati ili tuweze sasa kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni muhimu sana kwa sababu tunatumia fedha pia za *World Bank*...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tupunguze sauti tafadhali.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sharti ambalo Benki ya Dunia imetupa ni kutokuanza ujenzi hadi tuwe na hati ya eneo husika kwa ajili ya kujenga chuo. Kwa hiyo naomba sana utusaidie katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lako la pili kozi gani au *level* gani ya mafunzo ya afya itatolewa, itakuwa ni ngazi ya cheti *(certificate)* pamoja na *diploma.* kwa hiyo tutaendelea kufanya kozi ya uuguzi lakini pia tutaongeza na kozi nyingine ambazo ni muhimu katika utoaji wa huduma za afya ikiwemo wataalamu wa maabara. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, Mheshimiwa Tecla Ungele nimewaona.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Hospitali ya Rufaa ya Bugando inazidi kukua siku hadi siku na pale kuna Chuo Kikuu cha Afya na kuna Chuo cha Afya. Je, Serikali ipo tayari sasa kuhamisha Chuo cha Afya katika Manispaa ya Ilemela ambayo imetenga eneo la ekari 20 karibu na hospitali mpya ya wilaya ambayo Serikali imejenga? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula nimpongeze sana kwa jinsi anavyowapambania wananchi wa Ilemela na ni kweli nataka kukiri kwamba chuo chetu cha afya ambacho kipo katika Hospitali ya Rufaa Bugando kipo ndani ya hospitali, lakini hospitali nayo wana Chuo cha Afya Kikuu, kwa hiyo Wizara tayari ilishaliona hili la kukihamisha Chuo cha Afya cha Mafunzo ya Kati kilichopo Bungando. Kwa hiyo, kwa sababu umekuwa ni Mbunge wa kwanza wa Mkoa wa Mwanza kutupa ofa ya eneo naomba nikuahidi kwamba tutakuja Ilemela ili kujenga Chuo cha Afya Ilemela, tuwaachie Bugando waweze kufanya upanuzi wa majengo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tecla.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ujenzi wa jengo la Chuo cha Uuguzi Nachingwea ulioanza mwaka 2022 ulitarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2022 lakini hadi leo bado haijakamilika, je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa chuo kile ili kuongeza idadi ya wauguzi na kupunguza *shortage* ama upungufu wa wauguzi nchini Tanzania? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia taarifa zangu kama Nachingwea ipo, kwa kweli Mheshimiwa Tecla amekuwa ni mfuatiliaji mzuri sana wa ujenzi wa Chuo cha Afya Nachingwea, lakini kwa sababu na yeye ni mwanataaluma wa kada ya wauguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kukiri ni kweli ujenzi umechelewa, lakini tumepata fedha hizi za Benki ya Dunia na tumeweka katika orodha yetu Nachingwea moja ya majengo ya kumaliza. Kwa hiyo, naomba nikuhakikishie na mimi tukimaliza Bunge nitafanya ziara Nachingwea kufuatilia ujenzi wa jengo hili ambalo lilikwama kwa muda mrefu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cosato Chumi, halafu Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Vyuo vingi vya zamani kikiwemo Chuo cha *COTC* Mafinga miundombinu yake imechakaa sana. Je, Serikali ipo tayari kuwa na mpango maalumu wa kufanya ukarabati mkubwa katika vyuo vya zamani kikiwemo Chuo cha *COTC* Mafinga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Cosato Chumi kwa swali lake la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli majengo au miundombinu ya majengo katika vyuo vyetu vya afya vya mafunzo ya kati yamechakaa na ndiyo maana sasa tumekuja na huu mpango mahususi wa kufanya ukarabati wa majengo katika vyuo vyetu vya afya, lakini naomba niseme tunakwenda awamu kwa awamu. Kwa hiyo, Mafinga nayo tutaifikia na tumeamua kabisa siyo tu tujenge majengo ya hosteli, lakini kubwa tuwe na *academic complex,* lakini jambo la pili ni kuweka *skills lab* kwa ajili ya kuongeza ujuzi ili kuweza kuzalisha wanataaluma wa kada za kati za afya wenye uwezo, ujuzi na stadi zinazohitajika katika utoaji wa huduma za afya kwa sasa hivi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta, baadaye Mheshimiwa Hawa.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inatambua vipi mchango wa wadau mbalimbali ambao wamekuwa wakijenga majengo katika Wizara ya Afya kwa mfano katika Mkoa wetu wa Iringa tunaye mdau ambaye ni Salim Asas - *MNEC* amejenga jengo la mama na mtoto, amejenga jengo la *ICU VIP*, amejenga jengo la damu salama na kajenga karakana ya viungo bandia na majengo mengine katika wilaya na vituo vyetu vya afya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kwa kufuatilia masuala ya afya katika mkoa wa Iringa, lakini ni kweli pamoja na jitihada za Serikali, tumekuwa pia tukiungwa mkono na wadau mbalimbali kwa ajili ya kujenga majengo ya kutolea huduma za afya. Nikifanya tathimini ya haraka haraka nchi nzima mdau ambaye namwona binafsi amejitolea kujenga majengo mengi ya huduma za afya kama alivyosema Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ni Mheshimiwa Salim Asas - *MNEC* wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nikuahidi sisi kama Wizara na Serikali kwa ujumla tutamuandalia tuzo maalumu Bwana Salim Asas - *MNEC* ili kuweza kumshukuru na kumpongeza kwa jitihada zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ili kumuunga mkono kwa sababu ametujengea karakana ya viungo bandia na sisi Wizara sasa hivi na mimi nikiwa Waziri mwanamke na ni mama, tumeona ipo haja ya kuongeza mkazo katika huduma za utengamao hususani kwa watoto wenye ulemavu. Kwa hiyo, karakana hii tutaifanya ni moja ya karakana kubwa za nchini kwetu ili kutengeneza viungo bandia kwa watoto wenye ulemavu na watu wengine wenye uhitaji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, Mheshimiwa Saashisha nimekuona.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na niishukuru Serikali tunacho chuo cha afya katika Mkoa wa Tabora ambacho kipo katika hospitali ya Kitete, changamoto iliyopo ni ukosefu wa vifaa vya kufundishia pamoja na wakufunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka vifaa vya kufundishia na wakufunzi ili tuweze kupata wahudumu wa afya waliyo na elimu bora? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, kwa swali lake zuri kuhusu Chuo cha Afya Tabora na nataka kukubaliana naye umuhimu wa kuwekeza kwenye vifaa tiba pamoja na wataalamu ili kuweza kuzalisha wataalamu wa afya wenye ujuzi.

Kwa hiyo, kwa upande wa vifaa tiba Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, aah samahani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia tutaomba tupate orodha rasmi kutoka kwa Mkuu wa Chuo Tabora ili tuone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kwa upande wa wakufunzi jana nilitoa maelekezo kwa Katibu Mkuu kupeleka wakufunzi katika vyuo vya afya, lakini nimempa angalizo badala ya kuchukua wakufunzi ambao ndiyo wamemaliza tu masomo yao ya vyuo vikuu, wachukue wakufunzi ambao tayari wana uzoefu wa kufundisha na kutoa huduma za afya ndiyo wawe wakufunzi katika vyuo vya kutoa huduma za afya lakini pia waangalie kama vyuo vikuu vinavyofanya wanachukua wakufunzi ambao wamepata *GPA* kubwa.

Kwa hiyo, hili jambo nimelisisitiza sana siyo tu kupeleka mtu aliyemaliza chuo kikuu mnampeleka akawe mkufunzi wa Chuo cha Afya, Hapana, lakini lazima tuwekeze kwenye wakufunzi wenye sifa na uwezo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye sekta hii ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kufahamu wananchi wa Kata ya Narumu wameandaa eneo kubwa na la kutosha kwa ajili ya kujenga kituo cha afya, lakini na Chuo cha Afya Narumu. Je, hauoni ni wakati sahihi sasa Serikali kuweka kwenye mpango kwa ajili ya kuandaa maandalizi ya kujenga Chuo cha Afya cha Narumu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Saashisha kwa swali lake la nyongeza, lakini kwa kazi nzuri anayofanya kwa wananchi wa Hai na tunaamini wananchi wa Hai wataendelea kumuunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la ujenzi wa kituo cha afya na chuo cha afya na Kituo cha Afya Narumu niombe kwanza kitangulie kujengwa kituo cha afya kabla hatujaja kuweka chuo cha afya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Wizara ya Afya kwa majibu haya ya maswali mengi ya Wabunge.

Tunaingia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, Mbunge wa Tarime Mjini, aulize swali lake.

Na. 587

**Kulipa Fidia au Kurejesha Maeneo ya Mlima Tarime Nkongore**

**MHE. MWITA M. WAITARA K.n.y. MHE. MICHAEL M. KEMBAKI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italipa fidia au kurejesha maeneo ya wananchi katika Mlima Nkongore yaliyochukuliwa na Jeshi la Magereza – Tarime?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, Mbunge wa Tarime Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha tarehe 11 Novemba, 2017 cha Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya kilichojadili masuala mbalimbali ya ulinzi likiwemo suala la kilimo haramu cha zao la bangi na uharibifu wa mazingira kwa kukata miti katika maeneo mbalimbali likiwemo eneo la Mlima Nkongore. Kupitia kikao hicho, eneo la Mlima Nkongore lilikabidhiwa kwa

Jeshi la Magereza kwa lengo kuuhifadhi na kuulinda ili kuepusha uharibifu wa mazingira kwa kukata miti na kilimo cha zao haramu la bangi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004, kifungu cha 58(1) na (2) kinazuia kufanya shughuli zozote zinazoweza kupelekea hifadhi ya mlima kuharibiwa. Hivyo kutokana na sheria hiyo, taratibu za umiliki maeneo ya milima zinazuia kumilikishwa mlima kwa mtu yeyote, hivyo hapatakuwepo na fidia au kurejeshwa kwa eneo la Mlima Nkongore kwa wananchi, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, eneo hili Mheshimiwa Michael Kembaki, ameuliza mara kadhaa huku Bungeni, amemchukua Mheshimiwa Diwani wa Kata husika yeye mwenyewe wamekaa kikao cha wilaya na mkoa wakakubalina eneo hilo lisirudishwe kwa wananchi, lakini lirudishwe kwa jamii ile nalipangiwe matumizi ya kijamii, tuna uhaba mkubwa wa ardhi. Je, yamkini inaonekana Wizara ya Mambo ya Ndani ndio kikwazo na ndio wanazuia huo mpango usitekelezwe. Nataka nijue sababu ya Wizara kukataa ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kule Tarime Vijijini eneo la Mwema na Kata ya Regicheri, eneo lingine wamechukua wakawapa JKT wanalima, halafu lingine wamezuia zaidi ya mwaka mzima hakuna shughuli inafanyika pale. Je, huu utaratibu wa kutwaa maeneo ya watu wa Tarime na kuyahodhi na watu wanakuwa na shida ya kilimo utaisha lini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu

maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Waitara, kwa niaba ya Mheshimiwa Kembaki, naomba kujibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mlima huu kurudishwa kwa jamii badala ya kusimamiwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, nimeeleza msingi wa uamuzi ule ilikuwa moja, ni kuhifadhi mlima ule, lakini pili ni kuzuia uharamu wa mazao yaliyokuwa yanalimwa kwenye eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Mbunge alikuja sasa sijui alikutana na nani waliopatana, lakini kwa msimamo wa Wizara na kwa msimamo wa Kamati ya Usalama ya Wilaya eneo lile lipo nchi ya uangalizi wa Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili, la Mheshimiwa Waitara, naona ni kama amechomekea Mambo ya Ndani, kama ni JKT basi ni la Wizara ya Ulinzi, nimshauri aandae swali la msingi ili liweze kujibiwa ipasavyo na Wizara yenye dhamana na ulinzi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mheshimiwa Esther Matiko, atafuatia.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa magereza mengi yana mwonekano wa kuchoka sana, kwa mfano Gereza la Mjini Lushoto.

Je, ni lini Serikali itafanya utaratibu wa kuyakarabati magereza yote yakawa na sura ya matumaini ndani na nje haidhuru kwa kuwatumia wafungwa hao hao kwa kufanya kazi za ujenzi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la msingi lilikuwa kutwaa eneo na kutumiwa na magereza, lakini ninaweza nikamjibu kwa sababu nina *background* kidogo ya

eneo hilo. Ninafahamu mpango wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni kujenga upya magereza kwenye maeneo ambayo hayana magereza, lakini pia kukarabati magereza ambayo yamechakaa na ukarabati huo umeenza katika maeneo mbalimbali ili kuboresha hali ya magereza hizo.

Kwa hiyo, nimpe uhakika Mheshimiwa Mbunge kwamba kadiri hali ya fedha itakavyoruhusu kwa maana ya bajeti magereza kama alivyorejea hilo la Lushoto, litakarabatiwa ili lilingane na hadhi kama ambavyo ameshauri, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nisikitike kwa majibu ya Serikali, baada ya ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mkuu wa Mkoa ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya ambaye ni Mwenyekiti wa Ulinzi na Usalama wa Wilaya, walikaa na wakakiri kwamba watalirejesha lile eneo kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa kwa majibu uliyotoa hapa eneo lilochukuliwa ni zaidi ya eka 100 na imeathiri zaidi ya kaya 67 na kwa kuwa magereza wanafanya shughuli za kilimo kwenye hilo eneo. Serikali haioni sasa kuna haja ya kupeleka Mradi wa *BBT* ili wananchi wa eneo lile waendelee kufanya shughuli zao za kilimo na kupata kipato? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua umuhimu wa wananchi kuwa na ardhi ya kutosha kwa ajili ya shughuli zao za kiuchumi kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameshauri, lakini kwa sababu uamuzi ulishafanyika na kwa sababu ya ujirani mwema pengine kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nchi, nishauri kwamba uongozi wa Magereza Mkoa

wa Mara, uwasiliane na utawala ngazi ya Halmashauri ya Mji wa Tarime ili kuona namna ambavyo kwa ujirani mwema wanaweza wakaishi kati ya magereza na wananchi ambao wanahitaji eneo kwa ajili ya hicho kilimo, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa. Kwa kujibu maswali hayo ya Waheshimiwa kwa niaba ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Sasa tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Tamima Haji Abass, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 588

**Sheria ya Makosa ya Ukatili wa Kijinsia**

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatunga sheria mahsusi kwa makosa ya ukatili wa kijinsia?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuombe radhi, swali namba 589 ndilo nipo nalo hapa, bahati mbaya niruhusu nilipate jibu la swali hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sheria ya Ndoa, Sheria ya Mtoto, Sheria ya Makosa ya Mtandao na Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu zina vifungu vinavyozuia makosa ya ukatili wa kijinsia na vifungu vinavyohusika na makosa ya ukatili wa kijinsia. Hata hivyo, Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Wizara nyingine na asasi za kiraia inafanya tathmini ili kubaini iwapo ipo haja ya kuwa na sheria mahususi ya ukatili wa kijinsia au tuboreshe sheria zilizopo. Tathmini hiyo ikikamilika, itasaidia Serikali kufanya uamuzi sahihi kuhusu

suala la kutunga sheria mahususi kwa makosa ya ukatili wa kijinsia au kuboresha sheria zilizopo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tamima Haji Abass.

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa majibu hayo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, ni kigezo gani cha kubainisha haja ya kuwa na sheria mahususi ya makosa ya ukatili wa kijinsia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa vitendo vya ukatili wa kijinsia vinazidi kushamiri nchini na sheria zipo, je, Serikali inatumbia nini kuhusiana na hali hiyo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vigezo gani vinafaa ili iweze kuandikwa sheria moja, nimejibu katika swali la msingi kwamba ni tathmini ya uzito au ukengeufu unaosababisha na mtawanyiko wa sheria hizi hususani zikishafanyika na Tume ya Marekebisho ya Sheria *then* Serikali inashauriwa ipasavyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge utupe nafasi kama Serikali kupitia Tume yetu ya Kurekebisha Sheria ambayo inahusisha wadau mbalimbali wakiwemo Wabunge tutapata msimamo wa pamoja wa namna ya kuliendea jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuendelea kushamiri kwa matendo ya ukatili wa kijinsia, nichukue nafasi hii kuiasa jamii kwa ujumla wake kuzingatia maadili ya jamii, kwa sababu karibu Tanzania ambayo ina mila, desturi, dini mbalimbali hakuna hata moja inayoruhusu mambo haya kufanyika, lakini maadamu yanafanyika kwenye jamii zetu, niiase pale inapotokea wahusika watoe taarifa kwenye vyombo vyetu vya usimamizi wa sheria ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kuwafikisha wahalifu hao kwenye mahakama zetu, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane na Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, je, ni lini Serikali itakarabati Mahakama za Mwanzo katika Tarafa ya Kipatimu, Miteja na Njinjo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naona lipo tofauti na swali la nyongeza kama unaweza sawa, kama hujaweza liachie. Mheshimiwa Naibu Waziri, unasemaje? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilijibu wakati nitakapo jibu swali la ujenzi wa Mahakama ambalo litafuta muda mfupi ujao.

**MWENYEKITI:** Sawa, Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona, Serikali itunge sheria haraka ili wabakaji waache ukatili huu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, sheria itatungwa lini anauliza hivyo. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza katika jibu la msingi kwamba zipo sheria maeneo mbalimbali ambazo yoyote kati ya sheria hizo inaweza ikatumika kuwadhibiti watu wanaofanya matendo ya ukatili wa kijinsia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nimshauri tu ikiwa mambo yamefanyika kwenye masuala ya mitandao tutatumia Sheria ya Mitandao, ikiwa amefanyiwa mtoto ipo Sheria ya Mtoto na masuala mengine, ninashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe.

Na. 589

**Serikali Kujenga Mahakama ya Wilaya ya Buhigwe**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya ya Buhigwe ili wananchi waweze kupata huduma?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Wilaya ya Buhigwe ni miongoni mwa mahakama 18 za wilaya zilizojengwa na Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023. Ujenzi wa mahakama hiyo umekamilika na wananchi wanaendelea kupata huduma za kimahakama katika Mahakama hiyo tangu mwaka 2023, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nichukue nafasi ya pekee kuishukuru Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutujengea Mahakama nzuri katika Wilaya yetu ya Buhigwe. Pamoja na ujenzi huo na huduma zimekwishaanza, nina maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Mahakama ya Mwanzo ya Muyama katika Tarafa ya Muyama majengo yake yamechakaa sana, ni lini Serikali itakarabati mahakama hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Tarafa ya Manyovu kijiografia ni tarafa kubwa ina eneo la utawala wa kata 14. Mwaka 2022 Serikali ilikubali kutujengea mahakama mbili; moja Manyovu na nyingine eneo la kimkakati katika Kata ya Janda. Lini Serikali inaaanza ujenzi wa mahakama hizo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa pongezi ambazo zimetolewa kwa Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kutokana na uboreshaji wa sekta ya Mahakama kama inavyoendelea katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umuhimu wa kukarabati Mahakama ya Muyama, nikiri tu kwamba Mahakama zetu za Mwanzo katika maeneo mbalimbali ikiwemo hii ya Muyama iliyopo huko Buhigwe, ni kweli mahakama hizi ni kongwe na ni chakavu zinahitaji ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga ni kuchagua na kulingana na uwezo wa kibajeti mwaka huu tumeweza kujenga Mahakama ya Mwanzo ya Manyovu. Naomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na jitihada zake za kutaka haki iwafikie wananchi wake atuvumilie pale hali ya bajeti itakavyoruhusu basi Mahakama ya Muyama itakarabatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tarafa kubwa hii ya Manyovu yenye kata 14 kuhitaji mahakama katika Kata ya kimkakati ya Janda ninaomba nilichukue ombi lake hili ili sekta ya mahakama iweze kuliingiza katika mpango mkakati wake, ili pale fedha zitakapopatikana eneo hili la Janda liweze kujengewa Mahakama ya Mwanzo, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mnazungumza kwa sauti kubwa. Unajua kuzungumza kwa sauti kwenye Bunge inaweza kuwa inahatarisha usalama wa Bunge, ninaomba mtulie kidogo.

Kuna swali la Mheshimiwa Kumba Ndulane, naomba ulijibu la mahakama halafu atakuja Mheshimiwa Shekilindi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la Mheshimiwa Ndulane aliyeuliza umuhimu wa karabati, kwa maana ya kukarabati Mahakama

zilizochakaa, tunalichukua hili na hivi sasa Mahakama ipo kwenye mkakati wa awamu ya pili ya ujenzi na ukarabati wa mahakama zote kongwe na pale ambapo bajeti itakavyoruhusu, kwa kweli nia ya Mahakama ni kukarabati mahakama zote ili zifikie kiwango cha kutoa haki kwa wananchi kwa mazingira ambayo niwezeshi yanaweza kutumia *ICT* na vitu kama hivyo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tuwe na matumaini, fedha zikipatikana Mahakama zetu zote zitakarabatiwa, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shekilindi nilimtaja au ni Mheshimiwa, upo nyuma sana huko sikuoni. Pale nyuma Mheshimiwa.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mpakate.

**MWENYEKITI.** Mheshimiwa Mpakate, halafu Mheshimiwa Ester.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Nalasi, Mahakama ya Nalasi, ni moja ya Mahakama ambazo ziliwekwa kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha unaondelea kuweza kujengwa. Ni lini ujenzi ule wa Mahakama ya Nalasi utaanza? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba katika Mkoa wa Lindi zipo Mahakama ambazo zipo katika mpango wa kujengwa upya na kukarabatiwa ikiwemo hii ambayo Mheshimiwa Mbunge ameirejea. Nimwahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba pale fedha zitakapopatikana mahakama hiyo itaweza kufanyiwa ukarabati, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shekilindi kumbe ulikuwa upande huu, halafu Mheshimiwa Ester ajiandae.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Mahakama ya Wilaya ya Lushoto ni ya zamani sana, lakini Serikali iliahidi kwamba itajenga mahakama ile. Nataka kujua ujenzi ule utaanza lini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu jinsi Mheshimiwa Shekilindi anavyofuatilia uimarishaji wa sekta ya mahakama katika wilaya yake hasa ukizingatia Wilaya ya Lushoto kipo pia Chuo cha Mahakimu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Mahakama ya Lushoto mwaka huu ipo kwenye bajeti, pale taratibu za manunuzi zitakapokamilika ujenzi wa Mahakama hiyo utaanza, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tunashukuru kwa ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Bunda maana tulipanga kwenye nyumba ya mtu kwa muda mrefu, tumeshaondoka na hilo tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna uchakavu wa Mahakama za Mwanzo hasa ambazo zimechakaa sana Mahakama ya Mwanzo Kabasa na Mcharo. Ni lini sasa mtahakikisha mtatukarabatia au kutujengea Mahakama za Mwanzo katika hayo maeneo niliyoyataja kwenye Jimbo la Bunda Mjini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa pongezi zilizotolewa na Mheshimiwa Bulaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa Mahakama ya Bunda ya Wilaya, nimweleze tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango wa mahakama ni kujenga na kukarabati. Kwa maana

ya juhudi zilifanyika sasa na hivi karibuni Mkoa wa Mara unafahamu Mheshimiwa Bulaya, ulijengewa *Intergraded Justice Centre* (Kituo Jumuishi cha Mahakama), zinajengwa Mahakama, zimejengwa Mahakama Butiama, imejengwa Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mahakama za Mwanzo, mwaka huu tutajenga Kinesi, Mugumu na tutajenga Lugangabilili. Kwa hiyo, pale fedha zitakaporuhusu mahakama uliyoitaja ya Kabasa na Mcharo zitaweza kujengwa wa upya au kukarabatiwa kulingana na kiwango cha uchakavu uliofikiwa, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ahmed Shabiby na Mheshimiwa Kalogeris, wote wawili nimewaona.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Mwanzo ya Gairo, ilipitishwa toka mwaka 2010 na ilipita kwenye bajeti, lakini mpaka leo bado haijajengwa, ni lini itajengwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema wakati najibu jibu la msingi, ni mpango wa sekta ya mahakama kuboresha mahakama zake, lakini hii inakwenda na uwezo wa kibajeti na upatikanaji wa fedha. Kwa Mkoa wa Morogoro, Mahakama ya Wilaya ya Ulanga na Mahakama ya Kilosa ipo kwenye mpango wa ujenzi, lakini pale fedha zitakaporuhusu, pale fedha zitakapopatikana Mahakama ya Gairo itazingatiwa pia, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Tunamalizia na Mheshimiwa Innocent.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Kata ya Bwakira Chini imo katika mpango wa bajeti ambao tunaumalizia mwezi

huu wa Juni, ni lini itajengwa kwa sababu muda wa bajeti na umeshakwisha?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Kalogeris kwamba Mahakama yake ya Bwakira Chini kama alivyosema imo kwenye mpango wetu wa ujenzi na hivi sasa taratibu za manunuzi zinakamilishwa na pale zitakapokamilishwa ujenzi huo utaanza mara moja, wala hautaathirika na kuhama kwa mwaka wa fedha, kwa sababu ni fedha za maendeleo zitaombewa Wizara ya Fedha na kuhamisha hizo hizo kutumika hata baada ya Julai, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Katiba na Sheria kwa majibu ya maswali hayo mengi ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Ngara, aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 590

**Ujenzi wa Kituo cha Forodha cha Mugoma**

**MHE. NDAISABA G. RUHORO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Forodha cha Mugoma?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya eneo au kituo kuteuliwa kuwa eneo la forodha na kuweza kufunguliwa kama Kituo cha Forodha mahali popote nchini kuna taratibu za kisheria ambazo inabidi zifuatwe. Taratibu hizo ni pamoja na kutangazwa na kuchapishwa kwenye Gazeti la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, kwa mujibu wa Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ya mwaka 2004, kifungu namba 11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tathmini na fidia kwa ajili ya kutoa eneo hilo lilishafanyika na sasa taratibu nyingine za kisheria zinaendelea na baada ya taratibu hizo kukamilika ujenzi utaanza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa majibu mazuri sana ya Serikali, majibu mazuri yanayotoka kwa Waziri mzuri, tunashukuru sana, nina swali moja la nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Vituo vya Forodha vya Kabanga na Murusagamba vinafungwa saa 1.00 jioni hali ambayo inasababisha adha ya wasafiri wa mabasi kutoendelea na safari zao na magari makubwa kusitisha safari zao kupeleka mzigo nje ya nchi na kufanya nchi ishindwe kutoza kodi na kufanya miji yangu ya mipakani kutokuchangamka kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni upi mpango wa Serikali wa kuruhusu vituo hivi vya forodha viweze kufanya kazi saa 24 ili kuweza kuhuwisha biashara ya mpakani?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu ametoa kama ushauri kwamba tunapofunga vituo hivi saa nne tunasababisha shughuli

zisifanyike kwa muda wote na kwa mantiki hiyo kwa kuwa hiki ni Kituo cha Forodha kinahusisha pande mbili tukifanya masaa 24 upande mmoja bila upande mwingine haitafikia lengo hilo ambalo limekusudiwa.

Kwa hiyo, tumepokea jambo hilo, tutawashirikisha wenzetu wa upande wa pili wa kituo hicho cha forodha ili kuangalia makubaliano ya pamoja ya kufanya kazi kwa saa 24 na tukishakubaliana pande zote mbili basi tutaweza kufanya hivyo ili lengo liweze kutimia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aloyce Kamamba.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka wa Muhange katika Wilaya ya Kankonko unaunganisha nchi ya Tanzania na Burundi na uwepo wa forodha katika mpaka huo utapelekea Serikali kuweza kuongeza kipato, lakini bahati mbaya eneo hilo mpaka sasa halijajengewa Kituo cha Forodha. Ni lini Kituo cha Forodha kitajengwa katika mpaka wetu wa Muhange? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia sana eneo hilo na Mbunge amefuatilia si tu Kituo cha Forodha bali amekuwa akifuatilia pia barabara inayoelekea eneo hilo. Tulikaa na Waziri wa sekta tumepokea jambo hilo kwa sababu ni barabara na kituo ambacho kinaelekea kwenye makao makuu mapya ya nchi ya Burundi na mimi napanga kufika katika eneo hilo ili kuweza kujionea.

Kwa hiyo, tumepokea tutalifanyia kazi na Mheshimiwa Mbunge tutakupa mrejesho ili uweze kuwaarifu na wananchi wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea Wizara ya Uchukuzi Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Ally Mhata.

Na. 591

**Ujenzi wa Reli Kusini**

**MHE. YAHYA A. MHATA K.n.y. MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza: -

Je, mpango wa ujenzi wa reli ya Kusini umefikia wapi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TRC* imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa reli ya *Standard Gauge* kutoka Mtwara – Mbamba Bay na matawi yake ya Liganga na Mchuchuma yenye jumla ya kilometa 1,000. Aidha, mradi huu ni mmoja wa mradi unaopendekezwa kupatiwa ufadhili wa fedha za maandalizi ya mradi kupitia Mfuko wa Miradi wa Nchi za Ukanda wa Kusini mwa Afrika *(SADC-PPDFA)* ambapo kwa sasa timu kutoka Benki ya Afrika Kusini *(DBSA)* ilikuja Tanzania kwa ajili ya kufanya uthibitisho wa nyaraka *(due diligence)* za mradi ili kuendelea na hatua zingine za upatikanaji wa ufadhili wa fedha zitakazotumika kumnunua mshauri elekezi atakayekuwa na jukumu la kupitia andiko, kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kumpata mwekezaji kwa utaratibu wa ubia baina ya sekta ya umma na binafsi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita na

majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri juu ya mradi huu wa ujenzi wa reli kutoka Mtwara hadi huko *Mbamba Bay. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa Serikali, kwa kuwa mmeamua ku-*engage private partnership* kushiriki katika mradi huu, mimi nawapongeza sana na naiomba Serikali iongeze jitihada ili reli hii iweze kufunguliwa na iwe mkombozi kwa wananchi wa Kusini hasa usafirishaji wa makaa ya mawe kutoka Liganga, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mhata kwa kutoa pongezi, wachache sana wakitendewa mambo mema wanasimama na kushukuru. Kwa hiyo nakushukuru sana Mheshimiwa Mhata kwa kuwa na moyo wa shukrani ambao utazidishiwa yaliyo mema zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mgaya nilikuta, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni umuhimu wa kutengeneza baadhi ya mabehewa kuweka mfumo wa ubaridi *(cold room)* katika reli ya *TAZARA* ili tuweze kusafirisha parachichi zetu na mazao ya mboga mboga yamfikie mlaji wa mwisho yakiwa na ubora? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Mgaya kwa sababu ni mdau mkubwa sana wa reli ya *TAZARA* na tukubali ukweli kwamba kwa sasa katika reli yetu na mabehewa yaliyopo hatuna *cold rooms,* lakini kila mtu anafahamu umuhimu wa ukuwaji wa

sekta ya parachichi katika mikoa ya Mbeya, Njombe, Iringa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa Wizara tunapokea ushauri huu na tunapokwenda kwenye hatua ya pili ya maboresho makubwa ya reli yetu kutoka Dar es Salaam mpaka Kapiri Mposhi tutaona namna ya kuweza kuweka hicho alichokizungumza cha *cold room*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Shangazi nilikuona na Mheshimiwa Kunambi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Serikali imeboresha miundombinu ya Bandari ya Tanga kiasi kwamba shehena zimeongezeka, lakini reli ya kutoka Tanga kwenda Dar es Salaam na kutoka Tanga kwenda Arusha bado ni chakavu sana, je, kuna mpango wowote wa kuboresha reli hii ili sasa shehena hii iweze kutoka kwa urahisi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Shangazi, Mbunge wa Mlalo na Katibu wa Bunge la CCM kwa swali lake kubwa na zuri la maslahi ya watu wa Tanzania na watu wa Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inao mpango mzuri na kabambe kwa sababu inatambua umuhimu wa upande wa Kaskazini kwanza kwenye utalii, kilimo pamoja na sekta nyingine, hivyo katika mwaka wa fedha 2023/2024 tumeshafanya kazi kubwa, tulishasaini mkataba wa kununua *materials* za kukarabati reli inayotoka Tanga kuelekea mpaka Arusha kilometa 533.

Kwa hiyo, mara baada ya kusaini mkataba huo katika mwaka wa fedha huu unaofuatia tunakwenda kuanza kutoa reli iliyokuwepo, tunataka tuweke reli nzito ambayo itakuwa na *capacity* ya ratilika 80 kwa *yard*, iliyokuwepo ilikuwa 45 kwa *yard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii reli iliyopo sasa hivi *speed* inayokwenda treni ni karibu *speed* ya 15 - 20 kwa saa moja, hivyo inawachukuwa muda mrefu sana kufika kwenye *destination* inayotakiwa. Tukifanya maboresho haya *speed* itaongezeka mpaka 75, kwa hiyo muda kama ilikuwa ni saa 12 tutakuwa tunatumia saa karibu nne. Kwa hiyo, habari njema hii kwa watu wa Kaskazini, Tanga na Watanzania kwa ujumla juu ya maboresho makubwa ya reli ya Kaskazini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunambi.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Uchukuzi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Mlimba usafiri wa reli ya *TAZARA* ndiyo usafiri unaotegemewa, sasa lini mpango wa Serikali katika kuboresha reli hii ikiendana sambamba na kuongeza mabehewa na *route* za safari ya reli hii kutoka Dar es Salaam kwenda Mbeya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, reli ya *TAZARA* kama inavyofahamika ilijengwa miaka 1975 baina ya Serikali tatu, China, Tanzania na Zambia na kipindi chote hicho *designed capacity* ilikuwa ni *metric tons* milioni tano, lakini kutokana na ubovu wa miundombinu hatukufikia lengo. Habari njema kutoka kwa daktari wa maendeleo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Tanzania amefanya kikao na Waziri wa Zambia pamoja na Rais wa China, hivi ninavyozungumza tupo kwenye hatua za mwisho za majadiliano, reli nzima inakwenda kufumuliwa upya. Moja, kuongeza uwezo wa reli wa kubeba mzigo, lakini pili tutaongeza mabehewa pamoja na vichwa vya kutosha ya mizigo na abiria. Kwa hiyo, Wana-Mlimba na watumiaji wote wa reli hii inayotoka Dar es Salaam mpaka Kapiri Mposhi kilometa 1,860 waendelee kusubiri habari hii njema ambayo inakuja kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Kiti.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umemalizika na sasa nina matangazo hapa.

Kwanza nitaanza na matangazo ya wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, kuna wageni 12 waliokaa Jukwaa la Mheshimiwa Spika ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Haki Jinai na Sekretarieti yake ambapo ni Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Chande Othman - Jaji Mkuu Mstaafu na Mwenyekiti wa Kamati ya Haki Jinai. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wa pili ni Mheshimiwa Jaji Mstaafu Joseph Sinde Warioba - Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais Mstaafu na Mjumbe wa Kamati. *(Makofi)*

Wengine ni *IGP* Mstaafu Balozi Ernest Mangu - Mjumbe wa Kamati, Dkt. Laurean Ndumbaro - Mjumbe wa Kamati, Profesa Edward Hosea - Mjumbe wa Kamati, Dkt. Yahya Hamad - Mjumbe wa Kamati, Ndugu Saada Makungu - Mjumbe wa Kamati, Ndugu Omari Issa - Mjumbe wa Kamati, Ndugu Reuben Shesha - Mjumbe wa Kamati, Ndugu Christina Maganga - Mjumbe wa Kamati, Ndugu Berious Nyasebwa – Katibu Msaidizi wa Kamati, Ndugu Salimu Msemo – Sekretarieti. *(Makofi)*

Wageni hawa wameambatana na wasaidizi wao wote, karibuni sana Wajumbe wetu pamoja na viongozi wa Haki Jinai katika Bunge letu. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni wageni sita wa Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa ambaye ni Naibu Waziri wa Madini, ambao hawa ni Wajumbe wa Halmshauri Kuu ya CCM kutoka Wilaya ya Longido, Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa ambaye ni mpiga kura wake kutoka Busanda, Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Yahya Ally Mhata ambao ni mshauri wake mambo ya siasa na Katibu wa Mbunge kutoka Nanyumbu, Mkoa wa Mtwara. *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, wapiga kura wake kutoka Bunda, Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula ambao ni shemeji zake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, wanamazingira kutoka Taasisi ya *Green Environment Tanzania*. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Kikundi cha Futa Machozi kutoka Ilala, Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni kumi wa Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, ndugu zake kutoka Kanisa la *Cross of Jesus of All People*. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Wanamaombi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 30 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Kwaya ya Wanaume wa Kanisa la Mlima Kola kutoka Dayosisi ya Morogoro, karibuni. *(Makofi)*

Mgeni mwingine wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati ni Mchungaji wa Kanisa la KKKT Wiloles kutoka Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Wageni 50 wa Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Kikundi cha Hodari 4M wanaojishughulisha na ulinzi kutoka Dodoma na Arusha. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Mrisho Gambo ambao ni wanafunzi 100 na walimu 10 kutoka Shule ya Msingi Lucky Vicent ya Jijini Arusha. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; kuna Ndugu Peter Raphael Ngao, Afisa wa Polisi Mstaafu kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni watatu ambao ni familia ya Ndugu Handre Benekto Kilatila kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni 12 ambao ni Kikundi cha *Tulia Group* kutoka Kata ya Bigwa, Mtaa wa Transfoma, Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Wanafunzi 59 na walimu sita wa Shule ya Msingi Tumaini kutoka Bariadi, Mkoa wa Simiyu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni wetu karibuni sana katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Pia tuna matangazo mawili, tangazo la kwanza Waheshimiwa Wabunge wote mnatangaziwa kwamba leo tarehe 11 Juni, 2024 kutakuwa na semina kama ifuatavyo, saa 5.00 asubuhi na saa 7.00 mchana, semina kuhusu mgawanyo wa majukumu ya mihimili ya dola nchini Tanzania na saa 7.00 mchana hadi saa 9.00 alasiri semina kuhusu mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Kurekebisha Mfumo wa Haki Jinai nchini na utekelezaji wake.

Waheshimiwa Wabunge, wote mnaombwa muhudhurie semina hizi muhimu sana. Semina hizi zote zipo leo tarehe 11 Juni.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine mnatangaziwa kuwa Ofisi ya Bunge inaanda *Grand Bunge Bonanza* kwa ufadhili wa Benki ya *CRDB*. Tamasha hilo linatarajiwa kufanyika siku ya Jumamosi tarehe 22 Juni 2024 katika uwanja wa Jamhuri Jijini Dodoma. Tamasha hilo litakuwa na ushindani kati ya timu za Bunge na wadau wengine katika michezo ya mpira wa miguu,

mpira wa kikapu, mpira wa pete na kuvuta kamba. Aidha, michezo ya mpira wa wavu, riadha, kukimbia na gunia, michezo ya bao, kufukuza kuku na kupenya kwenye mapipa itahusisha Waheshimiwa Wabunge na watumishi. Mnakumbushwa kuendelea kufanya mazoezi ili kushiriki kikamilifu katika bonanza hilo.

Vilevile kama ilivyokuwa kwenye bonanza la mwaka jana, *Grand Bunge Bonanza* litakuwa na tafrija ya jioni yenye burudani mbalimbali kutoka kwa wadau wetu, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge wote na watumishi mnasisitizwa kushiriki tafrija hiyo muhimu na kwa wale watakaopenda kutoa burudani kuendelea na maandalizi.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo yetu kwa leo na kwa vile hatuna ratiba nyingine naahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 4.57 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 12 Juni, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*